

**Mchungaji, Kanisa la T.A.G MWENGE,
Mwenyekiti wa CASFETA,
Wahitimu katika mahafali haya,
Mabibi na Mabwana.**

**HOTUBA YA MAHAFALI YA WANAFUNZI WA
KIDATO CHA NNE - CASFETA ILIYOTOLEWA NA
B.O. SWAI (BIBI) KATIBU TAWALA MKOA WA
DARES SLAAM TAREHE 13 SEPTEMBER, 2008**

Shalom,

Mchungaji,

Najisikia kubarikiwa kupewa nafasi ya kushiriki katika mahafali haya ya wana CASFETA wa mwaka 2008. ninashukuru sana kwa kunialika. Nilipopata mwaliko huu nilijiuliza hivi niseme nini kwa watu waliokatika mazingira yenu. Mmesoma na kuchoka, kusomeshwa tena haifai kwani akili haina matunda tena. Hata hivyo inabidi niseme tu walau kuwapongeza na kuwatia moyo hivi.

Siku ya leo ni ya muhimu sana kwa wana- CASFETA kwani ni hatua moja katika safari ya maisha yenu. Siku mlipoanza masomo yenu ya Sekondari ilikuwa kama ndoto kuiona siku hii. Miaka minne au sita si mingi lakini katika maisha ya shule ni safari ndefu sana, kwa sababu inahatari, ni ngumu na ina vikwazo vya kila aina. Wengine walikwama katika ada mavazi au fedha za mfukoni. Wengine hawakupata kibali kwa waalimu au wenzao, wengine mikiki ya ujana, wengine afya mbaya, wengine ugumu wa masomo wengine mazingira magumu ya nyumbani, ili mradi kila mtu alikuwa na pito lake. Katika mazingira ya aina hii kuweza kufikia hatua hii salama inastahili pongezi nyingi na mimi ninawapongeza sana na kuwatakia ushindi katika maisha yajayo.

Mchungaji na wanaCASFETA,

Kwa mujibu wa imani yetu ni kuwa tunalo tumaini kuu, kwakuwa mwanzilishi wake alishinda na

ametuachia kielelezo kwahiyo hatuna budi kushinda na sisi. Vijana hawa walipokuwa pamoja walikuwa wanainuana na kutiana moyo kwa kuwa walikuwa kundi moja. Huko mnakokwenda pengine msipate ushirika kama huu, mliokuwa nao wakati mnasoma. Hata hivyo mtegemeeni kiongozi mkuu wa imani yetu, yeye hata waacha, wala kuwapungukia endapo mtamtegemea.

Huko duniani kuna taratibu zake na kanuni zake tofauti na maisha ya shuleni. Jipangeni kujifunza kila siku. Chagueni yaliyo mema, jitengeni na mabaya. Ujana ni hatua muhimu sana katika maisha ukichezea tu umepoteza mtaji mkubwa sana wa maisha. Fikiri kwa makini sana maamuzi yako. Kila uamuzi unaofanya unaathari siyo kwako tu na hata jamii yako. Usidhani kuwa ni wewe tu utapata hasara, bali wako watu wengi sana ambao wataathirika kutokana na maamuzi yako. Shida ya muda mfupi isikufanye

kufanya maamuzi mabaya yakakupotezea mwelekeo wa maisha milele.

Nikushauri hivi; jiulize nafasi yako ni ipi katika mustakabali wa maisha yako na ile ya jamii ni ipi? Tena kutokana na mazingira yanayokuzunguka, ujuzi na uzoefu ulio nao unaweza kufanya nini binafsi kwa ajili ya maisha yako mwenyewe au kwa jamii nyingine.

Sisi tumepewa utume na Bwana wetu kuwa nuru na taa ya ulimwengu, tena tumegizwa kutafuta roho zilizopotea. Je, unadhani ukipewa mtihani leo utapata alama ngapi? Tumia ujana wako vizuri, achana na uovu na kulalamika, uwe mkweli na mwenye msimamo. Tumia raslimali na fursa vizuri, uishi kwa faida. Hakikisha unakuwa msaada kwa wengine siyo tatizo, usipende kupewa kila siku, bali sema nitoe nini kwa ajili yako Mungu. Jiwekee malengo ya maisha, tena jifunze kwa watu waliofanikiwa.

Mchungaji na wana CASFETA,

Nimeeleza mengi, sasa napenda kuwapongeza tena na kuwatakia maisha yenye mafanikio huko mwendako. Baada ya kusema haya nawashukuru kwa kinisikiliza.

Asanteni sana na Mungu awatunze.